

HALMASHAURI YA MANISPAA YA UBUNGO
BARUA ZOTE ZITUMWE KWA MKURUGENZI WA MANISPAA

Simu Na: 022296341
Tovuti: www.ubungomc.go.tz
Email: info@ubungomc.go.tz



MKURUGENZI WA MANISPAA
MANISPAA YA UBUNGO
S.L.P. 55068
DAR ES SALAAM
27/-02- 2019

TAARIFA KWA UMMA NA VYOMBO VYA HABARI

HALMASHAURI YA MANISPAA YA UBUNGO IMEPITISHA BAJETI YA **TSHS. 84,698,016,720.80** KWA MWAKA WA FEDHA **2019/2020**. BAJETI HIYO IMEGUSA SEKTA ZOTE MUHIMU YAANI ELIMU, AFYA, MAJI, ARDHI NA MIPANGO MIJI NA MIUNDOMBINU KWA UJUMLA.

KATIKA MWAKA WA FEDHA **2019/2020** HALMASHAURI YA MANISPAA YA UBUNGO INATARAJIA KUPOKEA FEDHA KIASI CHA **TSHS. 65,543,407,633.00** KAMA RUZUKU KUTOKA SERIKALI KUU NA **TSHS. 18,404,609,088.00** IKIWA NI FEDHA ZA MAKUSANYO YA NDANI.

RUZUKU KUTOKA SERIKALI KUU INAJUMUISHA MISHAHARA, MATUMIZI YA KAWAIDA NA MIRADI YA MAENDELEO. VILE VILE KATIKA BAJETI YA MWAKA **2019/2020** WANANCHI WANATARAJIA KUCHANGIA KIASI CHA **TSHS. 750,000,000.00** KATIKA MIRADI YOTE ITAKAYOKELEZWA KWA MWAKA **2019/2020** SAWA NA ASILIMIA 1% YA BAJETI YA MANISPAA.

VIPAUMBELE VYA BAJETI YA MWAKA 2019/2020 NI KAMA IFUATAVYO:

- 1) KUBORESHA MAZINGIRA YAKUTOA HUDUMA KWA JAMII KWA KUJENGA OFISI ZA HALMASHAURI YA MANISPAA YA UBUNGO MTAA WA MJI MPYA AMBAPO KIASI CHA **TSHS. 700,000,000.00** ZIMETENGWA KATIKA BAJETI YA MWAKA 2019/2020.
- 2) KUWA NA HOSPITALI YA WILAYA **TSHS. 250,000,000.00**
- 3) UJENZI WA MACHINJIO **TSHS. 250,000,000.00**
- 4) UJENZI WA SOKO LA MBEZI **TSHS. 300,000,000.00**
- 5) KUIMARISHA UTAWALA BORA NA KULIPA KIINUA MGONGO KWA WENYEVITI WA SERIKALI ZA MTAA WANAOMALIZA MUDA WAO **TSHS. 25,000,000.00**

- 6) KUONGEZA MAPATO KWA KUBORESHA MIUNDOMBINU YA UKUSANYAJI, KUBUNI VYANZO VIPYA; UANZISHAJI WA STENDI MPYA MLOGANZILA NA MSUMI, UANZISHAJI WA MASOKO MAPYA **TSHS. 1,778,000,000.00**
- 7) KUONGEZA KIWANGO CHA UZOAJI TAKA NGUMU, KUNUNUA VIFAA VYA UBEBAJI TAKA, MAGARI, VIFAA VYA USAFI WA MAZINGIRA KULIPA GHARAMA ZA USAFI NA MITAMBO **TSHS3,029,565,841.96**
- 8) UJENZI WA MABWENI YA WASICHANA NA WAVULANA SHULE YA SEKONDARI GOBA **TSHS. 80,000,000.00**
- 9) KUTOA MIKOPO KWA VIKUNDI VYA WANAWAKE, VIJANA NA WALEMAVU **TSHS. 1,384,460,908.80**
- 10) KUPIMA MAENEO YA UMMA, KUTOA HATI MILIKI NA KUTWAA MAENEO KWA AJILI YA MIRADI YA UWEKEZAJI NA UJENZI WA HOSPITALI YA WILAYA **TSHS. 1,494,379,999.9**
- 11) KUBORESHA NA KUJENGA MIUNDOMBINU YA ELIMU MSINGI NA SEKONDARI KWA KUJENGA MADARASA, VYOO, OFISI ZA WALIMU, NYUMBA ZA WALIMU NA UJENZI WA BWENI SHULE YA SEKONDARI GOBA **TSHS. 1,168,000,000.00**

IMETOLEWA NA;

**KITENGO CHA HABARI NA UHUSIANO
HALMASHAURI YA MANISPAA YA UBUNGO**